

# JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBITI



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. AB.13/91/01A/VOL.5/79

03 Oktoba, 2023

## YAH: TANGAZO LA NAFASI 40 ZA KAZI YA MUDA YA KUKUSANYA MAPATO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBITI.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti, anapenda kuwatangazia Wananchi wenye sifa kuomba nafasi za kazi za mkataba za kukusanya mapato ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti kama ifuatavyo;

### 1. MKUSANYAJI WA MAPATO YA HALMASHAURI - NAFASI 40

#### A: SIFA ZA MWOMBAJI ;

- Awe raia wa Tanzania
- Awe mwaminifu, mwadilifu na mzalendo kwa kazi.
- Awe na umri kuanzia miaka 18 hadi 45
- Awe tayari kufanya kazi mahali popote ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti
- Awe anajua kutumia vyema simu janja (Smartphone)
- Awe na elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea
- Wenye mafunzo ya Astashahada, Stashahada na Shahada katika fani za Utawala, Serikali za Mitaa, Uhasibu, Ununuzi, Sheria, Maendeleo ya Jamii, Kilimo na Mifugo watapewa kipaumbele.

#### B: MAJUKUMU YA KAZI ;

- Kukusanya mapato na ushuru kupitia Mashine ya POS
- Kuwasilisha makusanyo yote Benki kwa wakati kulingana na sheria ya fedha
- Kutunza vitendea kazi na taarifa zinazohusu makusanyo

#### C: MALIPO ;

- Malipo ni Tsh. 200,000 kwa mwezi

#### D: MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE ;

- Waombaji wote waambatishe nakala ya Cheti cha kuzaliwa

- Nakala ya vyeti vya Taaluma
- Wasifu binafsi wa Muombaji - CV na picha 2 passport size ya hivi karibuni
- Barua ya utambulisho kutoka ofisi ya Serikali katika eneo analoishi muombaji
- Kitambulisho cha Nida au namba ya Nida
- Nakala ya Cheti cha kidato cha nne na kuendelea (Wasifu - CV).
- Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **16/10/2023** saa **9:30** Alasiri
- **Maombi yote yawasilishwe masijala ya Mkurugenzi Mtendaji au yatumwe kupitia anuani ifuatayo;**

Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti,  
132, Barabara ya Hande  
S.L.P 33  
61882 KIBITI - PWANI

Limetolewa na;

Hemed S. Magaro  
Mkurugenzi Mtendaji (W)  
Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti.

MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
YA KIBITI  
S.L.P 33  
KIBITI-PWANI

Nakala:-

“ Mbao zote za Matangazo,  
Ofisi zote za Umma,  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBITI.**